

SHULE YA SEKONDARI DOMA,
S.L.P. 6054,
MOROGORO.
MOB: 0717 638 178/0758 370 272
18/12/2020.

KUMB.NA

Jina la mwanafunzi

.....

S.L.P. 6054,
MOROGORO.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DOMA WILAYA YA
MVOMERO MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021**

1.0 Utangulizi:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na **kidato cha kwanza** katika shule ya **Sekondari Doma** kwa mwaka **2021**.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe 11/01/2021. Na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za Shule

(a) Sare ya shule hii ni **Shati jeupe mikono mifupi na suruali** kwa wavulana na **shati jeupe mikono mifupi na sketi** kwa wasichana.

Maelezo ya mshono **rinda box kwa wasichana na suruali yenye marinda mawili kwa wavulana.**

(b) Rangi ya Hijab ifanane na Sare za shule **iwe nyeupe**.

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta nyekundu kwa wavulana na wasichana na T-shirt nyekundu

2.2 Daftari, kalamu na Mkebe wa hesabu.

2.3 Mahitaji mengine ya kibinadamu (kama yapo yatajwe)

- *Rangi ya sare kwa suruali na sketi ni kijani.*
- *Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba kwa wote.*
- *Soksi nyeupe kwa wote.*
- *Sketi iwe ndefu ivuke magoti.*
- *Suruali isibane na iwe na "Turn up" chini.*
- *Daftari 9 (Tisa) kwa wote (Counter book).*
- *Mkanda mweusi kwa wavulana.*
- *Sketi mbili (02) na mashati mawili (02) wasichana*
- *Suruali mbili (02) na mashati mawili (02) wavulana.*

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

3.1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na-25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya Msingi yafuatayo:

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- (g) Kuvalaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ufukuzwe shule.

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji, Ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyा.
4. Uvutaji bangi.
5. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
6. Kupigana na kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochaea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

"KARIBU SANA KATIKA SHULE HII"


.....

EDWARD .L. MULAMBO

MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
DOMA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 6054
MOROGORO